

Kibanzi na Boriti ni nini kama tunavyosoma kwenye biblia?

Kibanzi Na Boriti, kwenye biblia vinamaanisha nini?

Boriti ni kipande kikubwa sana cha mbao, kinaweza kikawa ni ki-gogo, au nguzo, au mbao yoyote pana..

Lakini kibanzi, ni kichembe kidogo sana cha mbao, kama mchanga, hata wakati mwingine kufikia kuwa kama vumbi la mbao ambalo ni ngumu sana kuliona. Hicho ndicho kibanzi.

Sasa Bwana Yesu alitoa mfano huo, wa picha ili kuweka msisitizo kile alichotaka kukisema, yaani katika hali ya kawaida, kama wewe huwezi kuona nguzo iliyosimama mbele ya macho yako inayokuzuia usione kabisa, utaona vipi vumbi la mbao lililo katika jicho la mwenzako?..Umeona moja kwa moja huo ni unafki..

Vivyo hivyo na sisi kabla hatujawahukumu watu, tuyachunguze maisha yetu Je! hayo wanayoyafanya Je, hayapo ndani yetu na sisi? Kabla hujamwambia Fulani acha usengenyaji, Je! na wewe si msengenyaji? Kama sivyo basi ni heri ukae tu kimya, kwasababu mistari ya juu yake inasema, kipimo kile kile tuhukumucho ndicho tutakachokuhumiwa na sisi.

Mathayo 7:1 "Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi.

2 Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa.

3 Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii?

4 Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe?

5 Mna fiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.

Bwana atusaidie sote tuyashinde hayo.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii **+255**

Kibanzi na Boriti ni nini kama tunavyosoma kwenye biblia?

789001312

Mada Nyinginezo:

<https://wingulamashahidi.org/ikabodi-maana-yake-ni-nini/>

KAMA MMOJA TU NDIO HIVI! SI ZAIDI 153?

UNYAKUO.

MKUMBUKE MKE WA LUTU.

CHUKIZO LA UHARIBIFU

Kibanzi na Boriti ni nini kama tunavyosoma kwenye biblia?

Israeli ipo bara gani?

*Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote
yatakapotimia...!!*

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp